KISWAHILI - CBC GRADE 3 TERM 2 EXAMS 2023

MASWALI

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Jibu maswali kwa kutamka

1. Taja vifaa viwili vya shambani.
2. Bendera yetu ina rangi ngapi?
3. Wanafunzi huketi kwenye nini darasani?
4. Mwezi wa kumi wa mwaka ni?
5. Mtu anayevua samaki anaitwaje?

Kusoma kwa sauti

Fipi na Feva ni marafiki. Fipi anakula papai na Feva anakula fenesi. kando ya Fipi na Feva kuna paka na panya. Fipi na Feva wanaulizana kama paka na panya wanafanana. Fipi anasema ndiyo, paka na panya wanafanana. Wote ni wanyama wadogo. Feva naye anasema hapana paka na panya hawafanani. Paka ni mkubwa kuliko panya.

SARUFI

Kamilisha kwa '-ake' na '-ao'

1. Mataifa _____
2. Mwalimu _____
3. Nyimbo _____
4. Tunda _____
5. Mashati_____

Kanusha

6. Alipika _____
7. Wanasoma _____
8. Watavuna_____
9. Alikula_____
10. Kilioshwa _____

Jibu maamkizi